JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA

## TALAKA



### 1.0 UTANGULIZI
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia. Aidha, Tume ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma.

### 2.0 MAANA YA TALAKA
Talaka ni hati inayotolewa na mahakama baada ya kujiridhisha kuwa ndoa husika haiwezi kurekebishika.
Kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa mamlaka ya kutoa talaka ni ya mahakama pekee. Aidha, Mahakama itatoa amri ya talaka baada kujiridhisha kuwa ndoa husika imeshindwa kurekebishika.

### 3.0 MASHARTI YA KUOMBA TALAKA
Mwanandoa yeyote haruhusiwi kuiomba mahakama kuvunja ndoa ikiwa ndoa hiyo haijatimiza muda wa miaka 2 tangu kufungwa kwa ndoa hiyo.
Hata hivyo Sheria ya Ndoa inawaruhusu wanandoa ambao hawajatimiza miaka 2 kuwasilisha maombi ya talaka kwa kuomba na kupata ruhusa ya ya kufungua maombi ya kuvunja ndoa bila ya kutimiza sharti hili kutoka mahakamani.
Wanandoa wataruhusiwa na Mahakama ikiwa itathibitishwa kuwa mwanandoa anayeomba ruhusa hiyo yuko katika hali ngumu ya mateso. Maombi hayo pia yanaweza kuwasilishwa mahakamani bila kupitia au baada ya kupitia baraza la usuluhishi la ndoa.

### 4.0 BARAZA LA USULUHISHI LA NDOA
Sheria ya Ndoa imempa mamlaka Waziri wa Katiba na Sheria kuanzisha Baraza la Usuluhishi la Ndoa katika kila kata. Vilevile, Waziri anaweza kukasimu mamlaka ya kuwa Baraza la Usuluhishi la Ndoa kwa kamati au baraza linalofanya kazi za Baraza la Usuluhishi la Ndoa katika jamii na endapo atajiridhisha lina uwezo na jamii imeridhia. Mwanandoa haruhusiwi kuwasilisha shauri la kuvunja ndoa bila
ya shauri hilo kuwasilishwa katika Baraza la Usuluhishi la Ndoa na na Baraza likajiridhisha kwamba limeshindwa kutatua mgogoro huo. Mahakama inaweza kutozingatia masharti haya ikiwa mume au mke (mjibu maombi):
- ametelekezwa na hana taarifa yoyote ya mwenzi wake;
- anaishi nje ya Tanzania na pia hakuna uwezekano wa mwanandoa huyo kurejea ndani ya muda wa miezi sita baada ya tarehe ya maombi;
- mjibu maombi hajafika kwenye Baraza la Usuluhishi la Ndoa baada ya kutakiwa kufanya hivyo;
- amefungwa kifungo cha maisha au kisichopungua miaka 5;
- ana ugonjwa wa akili usio tibika.

Baraza linaposhindwa kusuluhisha mgogoro wa wanandoa, linatoa hati yenye mapendekezo yatakayowasilishwa mahakamani kuhusiana na mgogoro huo.

Uwakilishi Katika Baraza la Usuluhishi la Ndoa Katika Baraza la Usuluhishi la Ndoa mawakili hawaruhusiwi kumwakilisha mwanandoa yeyote wakati wa kuendesha shauri la mgogoro wa ndoa. Hata hivyo ndugu wa wanandoa anaweza kumwakilisha mwanandoa ikiwa Baraza la Usuluhishi la Ndoa limetoa ruhusa ya kufanya hivyo.

### 5.0 USHAHIDI KUWA NDOA HAIREKEBISHIKI
Suala la msingi ambalo mahakama hujielekeza katika mashauri ya kuvunja ndoa ni kuwa ndoa haiwezi kurekebishika. Masuala yafuatayo yatachukuliwa kama ushahidi katika kuthibitisha kuwa ndoa hairekebishiki:-
- mjibu maombi kushikwa ugoni zaidi ya mara moja;
- unyanyasaji wa kijinsia;
- ukatili wa kiakili au wa kimwili kwa mwombaji au watoto;
- kutengwa kwa mwanandoa;
- kutelekezwa kwa mwombaji kwa muda usiopungua miaka 3 ikiwa mahakama itajiridhisha ni makusudi;
- utengano kwa wanandoa kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu;
- kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka mitano na kwa kuangalia aina ya kosa la jinai;
- Ugonjwa wa akili uliothibitishwa na madaktari wasio pungua 2 mmoja akiwa ni mwenye taaluma ya magonjwa ya akili watako thibitisha hakuna matumaini ya kupona; au
- Kubadili dini

### 6.0 MALEZI NA MATUNZO YA WATOTO
Sheria ya Ndoa imeweka utaratibu wa kuwalea na kuwatunza watoto baada ya talaka. Mahakama inaweza kutoa haki ya malezi ya mtoto kwa baba au mamana enddapo kuna mazingira maalum yasiyofaa kwa mzazi yeyote kupewa mtoto, mtoto atalelewa na ndugu yeyote au jumuiya ambayo malengo yake ni ustawi wa mtoto. Katika kuamua haki ya malezi ya mtoto apewe baba au mama, kipaumbele kitakuwa ustawi wa mtoto na Mahakama itazingatia matakwa ya wazazi wa mtoto, matakwa ya mtoto ikiwa ana umri wa kuweza kueleza mawazo yake na mila na utamaduni wa jamii ambayo wadaawa wanaishi.

Kutakuwa na dhana kanushi kwamba ni vizuri mtoto wa chini ya miaka saba akalelewa na mama yake. Hata hivyo katika kuamua kama dhana hiyo inatumika katika mazingira ya kesi yoyote husika, mahakama itazingatia kutokuathiri maisha na ustawi wa mtoto kwa kubadili malezi.

### MGAWANYO WA MALI ZA WANANDOA
Mahakama ina mamlaka ya kugawa mali ya wanandoa iliyopatikana kwa nguvu zao au kuamuru kuuzwa kwa mali hiyo kugawanya mapato hayo. Katika kufanya hivyo mahakama itajielekeza katika
- Mila za jamii ambayo wanandoa wanatoka;
- Kiwango cha mchango wa mwanandoa katika kupatikana mali ya wanandoa;
- Madeni wanayodai wanandoa ikiwa yaliingiwa kwa manufaa ya pamoja;
- Mahitaji ya watoto wadogo kama wapo

### 10.0 HITIMISHO
Taasisi ya ndoa ni muhimu katika jamii, kutokana na umuhimu huo Sheria imeweka taratibu kadhaa za kufuatwa ili kuivunja ndoa hiyo na kutoa utaratibu baada ya ndoa kuvunjika kwa kuangalia mali za wanandoa na malezi ya watoto.


**Kwa Maoni, wasiliana na Tume kupitia anuani ifuatayo :**

**Katibu Mtendaji,**
**Tume ya kurekebisha Sheria Tanzania ,**

**Jengo la Taaluma Na. 1,**
**Barabara ya Mkalama**
**S.L. P 1718**
**DODOMA**
**TANZANIA**

**Barua pepe: lrct@lrct.go.tz**
**Tovuti: www.rlct.go.tz**